

KSh. 4,000

UTOHOZI FONOLOJIA WA MANENO MKOPO YA KISWAHILI
KUTOKA KIINGEREZA

DORCAS MUENDI MUSYIMI
C82/24377/2011

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA SHULE YA FANI NA SAYANSI ZA
JAMII ILI KUTOSHELEZA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU
KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA




Musyimi, Dorcas Muendi
*Utohozi fonolojia wa
maneno mkopo ya*



KENYATTA UNIVERSITY LIBRARY

UNGAMO


Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa minajili ya shahada au stashahada katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi:  Tarehe: 8/9/17

Dorcas Muendi Musyimi

C82/24377/2011

Tasnifu hii imewasilishwa kutahiniwa na kupitishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Kenyatta.


Sahihi:  Tarehe 08/09/2017

Dkt. Leonard. M. Chacha

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta

na

Sahihi:  Tarehe: 12/09/2017

Dkt. Jacktone. O. Onyango

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia wafuatao: Mume wangu

Dkt David Musyimi, ulinifaa kwa hali na mali huku ukijitolea kunipa msukumo wa kutimiza ndoto yangu ya usomi. Changamoto zilipokithiri ulinihimiza nijitahidi zaidi. Ukingoni tumefika pamoja. Mola akubariki.

Wanangu: Wana wa kujivunia: Janet Ndanu na Joshua Muuo. Kazi ya utafiti iliponibana mlinielewa na kunihimiza kutokata tamaa. Mungu awajalie kusoma hadi kiwango cha juu zaidi. Asanteni

Baba mzazi: Stephen Kitivi Maweu, maneno yako yalikuwa kwamba:

"Aliyeanza kusoma na kukosa kukamilisha usomi wake ni sawa na yule hajawahi kusoma". Kauli hii ilinitia shauku ya kuendelea hata nilipolemewa. Hatimaye matunda yake yamedhihirika. Asante kwa maneno yako ya hekima na ya kunitia moyo. Rabuka akubariki.

SHUKRANI

Namshukuru Mola kwa kunijalia afya njema na uwezo wa kuweza kuikamilisha kazi hii.

Shukrani kwa sahibu mume wangu Dkt David Musyimi, muungwana kwa vyovyote vile. Ulikuwa nami bega kwa bega katika kuhitimisha utafiti huu. Uliniunga mkono na ukajitolea bila malalamiko yoyote. Asante.

Shukrani nyingi ziwaendee wanetu Janet Ndanu na Joshua Muuo kwa uvumilivu wenu nilipokuwa nimezama masomoni.

Nawatolea shukrani zisizo na kipimo manahodha wa kazi hii Dkt L. M. Chacha na Dkt J. O. Onyango kwa kunielekeza na kuwa na subira nami katika safari hii ya kiakademia tangu mwanzo hadi tamati. Mlijitolea na kunikosoa kwa uelewavu uliokithiri mipaka. Uvumilivu wenu kwangu ulinipa mshawasha wa kuendelea kuzama kila nilipohisi kwamba nalemewa. Kwa hayo na mengine ambayo Mungu aliyaona katika siri, Mola awazidishie baraka zake ili mwendelee kuwaongoza wengine kwa moyo uo huo. Aonaye kwa siri atawajibu kwa wazi.

Sitawasahau wengine waliochangia katika kufanikisha kazi hii kama vile: Prof King'ei-Chuo Kikuu cha Kenyatta, Prof Mukuthuria-Chuo Kikuu cha Maasai Mara, Bi Sarah Ngesu-South Eastern Kenya University. Wataalamu hawa walinifaa sana katika kuiteua mada hii. Asanteni sana.

Mchango wa ndugu zangu, mashemeji na marafiki hautasahaulika kamwe. Walionikumbuka katika maombi ama wakanisaidie kwa chochote kile, Mola awazidishie baraka zake. Kwa hakika, walionitia shime ni wengi na siwezi nikawataja wote.

YALIYOMO

UNGAMO.....	ii
TABARUKU	iii
SHUKRANI.....	iv
YALIYOMO	v
ORODHA YA ISHARA, ALAMA NA VIFUPISHO	x
ORODHA YA MAJEDWALI	xi
ORODHA YA VIELELEZO	xii
MAELEZO YA ISTILAHU MUHIMU	xiv
IKISIRI.....	xv
SURA YA KWANZA	1
UTANGULIZI	1
1.0 Usuli	1
1.1 Suala la Utafiti	4
1.2 Malengo ya Utafiti	5
1.3 Maswali ya Utafiti.....	5
1.4 Sababu za Kuchagua Mada	6
1.5 Upeo na Mipaka.....	7
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada	9
1.7 Misingi ya Nadharia	16
1.7.1 Nadharia ya Fonolojia Leksia.....	17
1.7.1.1 Sheria	17

1.7.1.2 Kanuni za Fonolojia Leksia	19
1.7.2 Nadharia ya Kanuni za Usilabishaji	26
1.7.3 Vigezo Vya PEGITOSCA	30
1.8 Maadili.....	32
1.9 Mbinu za Utafiti.....	33
1.9.1 Mbinu za Ukusanyaji Data	34
1.9.1.1 Kusikiliza.....	34
1.9.1.2 Kushiriki	35
1.9.1.3 Eneo la Utafiti.....	36
1.9.2 Vifaa vya Utafiti	37
1.9.3 Uteuzi wa Sampuli.....	37
1.9.4 Uchanganuzi wa Data	39
1.10 Hitimisho	39
SURA YA PILI	41
MFUMO WA KIFONOLOJIA WA LUGHA YA KISWAHILI NA	
KIINGEREZA	41
2.0 Utangulizi	41
2.1 Vigezo vya Fonolojia ya Kiswahili	42
2.1.1 Fonimu za Kiswahili.....	42
2.1.1.1 Konsonanti za Kiswahili.....	43
2.1.1.2 Vokali za Kiswahili	47
2.1.2 Silabi za Kiswahili.....	48

2.1.2.1 Maumbo ya Silabi za Kiswahili.....	49
2.1.2.2 Aina za Silabi za Kiswahili.....	51
2.2 Vigizo vya Fonolojia ya Kiingereza.....	52
2.2.1 Fonimu za Kiingereza.....	53
2.2.1.1 Konsonanti za Kiingereza.....	53
2.2.1.2 Vokali za Kiingereza	56
2.2.2 Silabi za Kiingereza.....	60
2.2.2.1 Maumbo ya Silabi za Kiingereza.....	64
2.2.2.2 Aina za Silabi za Kiingereza.....	67
2.3 Hitimisho	70
SURA YA TATU	73
TARATIBU ZA UTOHOZI FONOLOJIA.....	73
3.0 Utangulizi	73
3.1 Utohozi Fonimu.....	74
3.1.1 Utohozi Vokali.....	74
3.1.1.1 Mabadiliko ya Vokali Pacha.....	75
3.1.1.2 Mageuko ya Vokali Pacha Kuwa Vokali Mbili.....	79
3.1.1.3 Udondoshwaji wa Vokali Ndefu	79
3.2 Utohozi Silabi	84
3.2.1 Uchopekaji wa Sauti.....	92
3.2.1.1 Uchopekaji Vokali Mwishoni mwa Neno	92
3.2.1.2 Uchopekaji Vokali Katikati mwa Neno.....	99

3.2.1.3 Kuongezeka kwa Idadi ya Silabi	101
3.3 Udumishaji wa Maumbo ya Maneno ya Mkopo.....	104
3.4 Ukopaji wa Maneno Mwambatano	105
3.5 Hitimisho	109
SURA YA NNE	111
UTATA NA UKUBALIFU WA MANENO YA MKOPO	
YALIYOTOHOLEWA	111
4.0 Utangulizi	111
4.1 Utata wa Maneno ya Mkopo ya Kiswahili kutoka Kiingereza	112
4.1.1 Udahiri wa Maneno ya Mkopo ya Kiswahili kutoka Kiingereza	112
4.1.2 Uzalishaji wa Maneno ya Mkopo zaidi ya Moja kwa dhana Moja	114
4.1.3 Utaratibu Maalum na Utohozi wa Maneno ya Mkopo	115
4.1.4 Utaratibu Sawa na Utohozi wa Maneno ya Mkopo.....	116
4.2 Ukubalifu na Ufaafu wa Maneno ya Mkopo ya Kiswahili.....	118
4.3 Hitimisho	119
SURA YA TANO	120
MUHTASARI NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ZAIDI	120
5.0 Utangulizi	120
5.1 Muhtasari	120
5.2 Matokeo ya Utafiti	122
5.3 Changamoto za Utafiti	125
5.4 Mapendekezo ya Utafiti Zaidi	126

MAREJELEO	127
KIAMBATISHO 1: ORODHA YA MANENO YA MKOPO	137
KIAMBATISHO 2: KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI KUTOKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA	143
KIAMBATISHO 3: KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI KUTOKA NACOSTI	144
KIAMBATISHO 4: KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI KUTOKA KWA KAMISHINA WA KAUNTI YA NAIROBI	145

ORODHA YA ISHARA, ALAMA NA VIFUPISHO

//	Unukuzi wa fonimu
o	Mofu kapa
#	Kuonyesha mpaka wa neno hivi kwamba: #_____nafasi katika mwanzo wa neno _____# nafasi katika mwisho wa neno
[]	Alama za kufungia vipashio kwa mujibu wa kanuni ya kufuta mabano, kwa mfano [[anatom][u]]→[anatomu]→#anatomu# kutokana na neno <i>anatomy</i>
+	Weka pamoja na
→	Kubadilika na kuwa
{ }	Unukuzi wa mofimu
/	Katika mazingira ya
R	Ni kiwakilishi cha kiwango cha kupendekeza kitajwa kupewa hadhi ya msamiati au istilahi.
X	Ni vitajwa
NACOSTI	National Commission for Science, Technology and Innovation
P, E, G, I, T, O, S, C, A	Ni herufi zinazounda formula ya PEGITOSCA.
K	Konsonanti
KIT	Kitangulio
KIF	Kifungio
KIL	Kilele
KIN	Kina
SI	Silabi
V	Vokali

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 2.1: Jozi finyu za Kiswahili	43
Jedwali 2.2: Konsonanti za Kiswahili	44
Jedwali 2.3: Namna ya Kutamka, Mahali pa Kutamkia na Mkao wa Glota	45
Jedwali 2.4: Utambulisho wa Vokali za Kiswahili	48
Jedwali 2.5: Vokali za Kiswahili	49
Jedwali 2.6: Maumbo ya Silabi za Kiswahili	50
Jedwali 2.7: Konsonanti za Kiingereza	54
Jedwali 2.8: Namna ya Kutamka na Mahali pa Kutamkia	55
Jedwali 2.9: Vokali Fupi	60
Jedwali 2.10: Vokali Pacha	61
Jedwali 2.11: Maumbo ya Silabi za Kiingereza	66

ORODHA YA VIELELEZO

SURA YA KWANZA

Kielelezo 1.1: Uundaji wa Maneno Kimsonge	19
Kielelezo 1.2: Mzunguko wa Sheria	21
Kielelezo 1.3: Uundaji wa Nomino kwa Kanuni ya Mzunguko Kamili	23

SURA YA PILI

Kielelezo 2.1: Konsonanti Sahili na Changamano za Kiswahili	47
Kielelezo 2.2: Maumbo ya Silabi za Kiswahili	51
Kielelezo 2.3: Aina za Silabi	53
Kielelezo 2.4: Konsonanti Sahili na Changamano za Kiingereza	56
Kielelezo 2.5: Umbo la Vokali Sahili	61
Kielelezo 2.6: Umbo la Vokali Pacha	62
Kielelezo 2.7: Maumbo ya Silabi za Kiingereza	68
Kielelezo 2.8: Silabi za Vokali Moja	69
Kielelezo 2.9: Silabi za Konsonanti na Vokali	70
Kielelezo 2.10: Silabi za Kina cha Umbo la Kilele na Kifungio	71
Kielelezo 2.11 Silabi za Kitangulio na Kifungio	71

SURA YA TATU

Kielelezo 3.1: Vokali Pacha kuwa Vokali Sahili	77
Kielelezo 3.2: Vokali Ndefu kuwa Vokali Fupi	81
Kielelezo 3.3: Vokali Ndefu kuwa Vokali Fupi katika Kuunda Silabi	84

Kielelezo 3.4: Kutobadilika kwa Vokali Ndefu	85
Kielelezo 3.5: Mkururo wa Konsonanti katika Kuunda Silabi	87
Kielelezo 3.6: Uchopekaji Vokali Mwishoni mwa Neno	94
Kielelezo 3.7: Silabi Funge kuwa Silabi Wazi	95
Kielelezo 3.8: Sheria ya Mzunguko Kamili	98
Kielelezo 3.9: Uchopekaji Vokali Katikati mwa Neno	101
Kielelezo 3.10: Kuongezeka kwa Idadi ya Silabi	103
Kielelezo 3.11: Umbo la Silabi Funge ya Kiingereza	105
Kielelezo 3.12: Umbo la Silabi Wazi ya Kiswahili	106
Kielelezo 3.13: Udumishaji wa Maumbo ya Maneno ya Mkopo	107
Kielelezo 3.14: Maneno ya Mkopo Mwambatano	108
SURA YA NNE	
Kielelezo 4.1: Ukosefu wa Udhahiri wa Maneno ya Mkopo	115
Kielelezo 4.2: Uzalishaji wa Maneno ya Mkopo zaidi ya Moja kwa Dhana Moja	116
Kielelezo 4.3: Maneno ya Mkopo yenye Maumbo Tofauti	118
Kielelezo 4.4: Utaratibu Sawa na Utohozi wa Maneno ya Mkopo	119

MAELEZO YA ISTILAHU MUHIMU

Fonolojia	Kiwango cha isimu ambacho huohambua mfumo wa sauti katika lugha fulani.
Leksikolojia	Taaluma inayochunguza jinsi manono mapya yanavyoingia katika jamii lugha ama kwa kukopa kutoka lugha nyingine au kuunda maneno mapya kutokana na lugha nyingine.
Lugha changishi	Lugha inayokopwa manono/lugha inayochangia maneno.
Lugha pokezi	Lugha inayokopa/lugha inayopokea maneno.
Maneno mageni	Maneno mkopo katika lugha yoyote ile.
Mtagusano	Hali ya lugha mbili kuathiriana kutokana na kutumika katika jamii moja.
Ukopaji	Kitendo cha kuhamisha kipashio fulani kutoka lugha moja na kukiingiza katika lugha nyingine.
Utohozi	Hali ya kuyapatia maneno yaliyokopwa matamshi au maandishi ya lugha pokezi.

IKISIRI

Utafiti huu umechunguza utohozi fonolojia wa maneno ya mkopo ya Kiswahili kutoka Kiingereza. Azima kuu ikiwa ni kuchanganua michakato ya kifonolojia inayofanikisha utohozi huo kulingana na fonolojia ya lugha pokezi. Pia, utafiti huu umebainisha ubadilishaji wa fonimu za Kiingereza hadi Kiswahili katika maneno mkopo yaliyoteuliwa. Isitoshe, utafiti umeangazie upungufu unaosababishwa na utohozi huu wa kifonolojia na kutoa mwelekeo wa jinsi upungufu huo unavyoweza kusuluhishwa. Mtafiti alitumia nadharia ya Fonolojia Leksia ambayo hushughulikia sauti za lugha pamoja na nadharia ya Kanuni za Usilabishaji ili kuchanganua suala la silabi. Isitoshe, mtafiti alitumia vigezo vya PEGITOSCA katika kutathmini ufaafu wa msamiati unaobuniwa kwa kutumia mbinu ya utohozi. Utafiti huu ulifanywa nyanjani ambapo mtafiti alipata maneno mkopo kutoka sajili ya taaluma ya teknolojia ya habari na mawasiliano, spoti hasa mchezo wa kandanda, dini, afya, usafiri na biashara. *Kamusi ya Karne ya 21 (Toleo la Pili)* iliyochapishwa na *Longhorn* (2013) ilitumiwa ili kuthibitisha kwamba maneno mkopo husika yalikuwa na asili ya Kiingereza. Pia, mtafiti alitumia *Kamusi ya Kiswahili Sanifu (Toleo la 3)* iliyochapishwa na TATAKI (2014) ili kuthibitisha usanifu wa maneno mkopo yaliyotumika. Utafiti huu ulifanywa maktabani kwa kupitia vitabu, tasnifu, majarida na huduma za mtandao ili kupata habari zaidi kuhusu maneno ya makopo. Mbinu za utafiti zilizotumiwa ni kushiriki na kutazama. Maneno ya mkopo yaliandikwa na pia yakarekodiwa. Data ilichanganuliwa kwa kufuata maswali ya utafiti na mihimili ya nadharia zilizotumikizwa kisha ikawasilishwa kwa njia ya maelezo na majedwali. Utafiti huu uliweka wazi michakato ya kifonolojia inayoongoza utohozi wa maneno mkopo kwa kutegemea lugha pokezi. Michakato hii ni uchopekaji wa sauti, udondoshaji wa vokali, ufupishaji wa vokali, ubadilishaji wa sauti, udumishaji wa maumbo na ubadilikaji wa maumbo ya silabi. Utafiti ulidhihirisha kwamba, ingawa mbinu hii ya uundaji wa msamiati ni faafu, huwa na utata kwani baadhi ya maneno ya mkopo si dhahiri na wala hayafuati utaratibu maalum na ulio sawa. Suluhisho la utata huu ni kwamba utohozi ufanywe kwa kufuata matamshi ya lugha lengwa wala si maandishi ya lugha chanzi. Matokeo ya utafiti huu yatachangia katika usomi wa Kiswahili, isimu za lugha kwa ujumla na kwa watafiti wa Isimu Historia. Mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe kwa kuzingatia matawi mengine ya isimu; sintaksia, mofolojia, semantiki na pragmatiki. Pia utafiti unaweza kufanywa kuhusu fonolojia arudhi ya maneno mkopo katika Kiswahili au katika lugha zingine. Mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe ili kuchunguza istilahi zote zilizowasilishwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi ya Kiswahili iwapo zina ufaafu kwa misingi ya kimataifa kama inavyopendekezwa na kanuni za PEGITOSCA. Aidha, utafiti unaweza kufanywa kuhusu istilahi zilizomo kwenye kamusi za Kiswahili na zitumiwazo na wahadhiri wa lugha ya Kiswahili wanapofunza isimu katika vyuo vikuu. Nadharia ya Usilabishaji inaweza kutumikizwa katika utafiti wa fonolojia wa lugha zingine ambazo hazina misingi wa Kibantu ili kuchunguza jinsi zinavyosilabisha maneno ya mkopo.